# KUMBUKIZI YA PROF. PADRI ZACHARIA SALIM MARKO MOCHIWA

*Anna Kishe*

## 1.0 Utangulizi

Maisha ya binadamu hapa duniani yametawaliwa na wakati. Miezi michache iliyopita kabla ya tarehe 11 Januari, 2008, tulikuwa tunamzungumzia Profesa Zacharia Mochiwa akiwa hai, sio mfu wala hayati. Ambapo tarehe 11 Januari alitajwa kama marehemu. Tarehe 20 Machi, 1946 alitajwa akiwa mtoto mchanga. Haya ndio maisha na hatua anazopitia binadamu yeyote yule. Mhubiri katika kitabu kitakatifu cha Biblia ameelezea nyakati na matukio mbalimbali yanayotawala maisha ya binadamu. *Mhubiri* 3:1-2,4 anasema:

> Kwa kila jambo kuna majira yake,
> Na wakati wa kila kusudi chini ya mbingu
> Wakati wa kuzaliwa na wakati wa kufa
> Wakati wa kupanda na wakati wa kung'oa yaliyopandwa
> Wakati wa kulia na wakati wa kucheka
> Wakati wa kuomboleza na wakati wa kucheza

Nia ya wasifu huu sio kuhubiri. Ninataka tufarijiane na kukumbushana kuwa tupo hapa duniani kwa muda tu. La muhimu zaidi ni kuwa wakati tutakapoondoka katika dunia hii tutakuwa tumeacha kumbukumbu gani? Japo mwenzetu Prof. Zacharia Mochiwa ameondoka katika dunia hii, ametuachia mengi mazuri ya kukumbukwa.

Zacharia Mochiwa anakumbukwa kama Padri na Profesa. Tutamwangalia Hayati Zacharia Mochiwa kama mwanataaluma mbobezi katika lugha ya Kiswahili na pia kama mchungaji au padri.

## 2.0 Mwanataaluma, Mfanyakazi wa Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA)

Profesa Zacharia Mochiwa alikuwa mtaalamu wa lugha ya Kiswahili aliyependa kuutumia ujuzi na utaalamu wake kwa vitendo. Raghba hii ilimsukuma kujiunga na Baraza la Kiswahili la Taifa. Profesa Zacharia Mochiwa alijiunga na Baraza la Kiswahili la Taifa Julai 1973 hadi Juni 1974. Alirudi tena BAKITA Aprili 1977 hadi 1978 akiwa Mchunguzi wa lugha, baada ya kuhitimu masomo ya shahada ya kwanza Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Alikuwa mtaalamu wa sarufi, mofolojia, semantiki na hata sintaksia. Kutokana na sifa hizi kazi ya uchunguzi aliifanya kwa umahiri mkubwa. Aliongoza mijadala mizito kuhusu tahajia, maana, matamshi na maandishi ya

Kiswahili na kuandika makala nyingi za kitaaluma katika uwanja wa sarufi na hata isimu jamii pia. Makala zake zimechapishwa katika jarida la BAKITA, "*Lugha Yetu*" na katika majarida mengineyo kama vile *Mulika, Kioo cha Lugha* n.k. Alikuwa mtetezi wa lugha ya Kiswahili na daima alishikilia kuwa lugha haiwi lugha bila sarufi.

**3.0 Mjumbe wa BAKITA**

Kutokana na utaalamu wa sarufi na umahiri mkubwa aliokuwa nao katika kutumia msamiati wa Kiswahili, mwaka 1979-1986 na 1999-2002 aliteuliwa kuwa mjumbe wa Kamati ya Kusanifu Lugha na Kamati ya Sarufi na Ithibati. Profesa atakumbukwa kwa mchango wake katika masuala ya sarufi na matumizi ya maneno ya Kiswahili. Profesa alikuwa hodari wa kuchagua maneno kufuatana na muktadha. Mara nyingi uchaguzi wake ulikuwa sahihi. Profesa alisisitiza matumizi ya lugha fasaha na sahihi. Katika makala zake nyingi alionesha jinsi ambavyo matumizi ya maneno yasiyo sahihi yanavyoweza kusababisha mgongano katika mawasiliano kiasi cha kuzusha vita.

Katika kamati ya kusanifu lugha, kwa hakika Prof. Mochiwa alikuwa hazina kubwa ya msamiati, hasa msamiati unaotokana na lugha za asili. Prof. Mochiwa alikuwa mahiri wa lugha yake ya asili - Kizigua. Alifahamu Kizigua katika viwango vyote, Kizigua cha ndani na cha nje. Kwa hali hii aliweza kupenyeza maneno mengi ya Kizigua katika msamiati wa Kiswahili. Neno "kitivo" ni miongoni mwa maneno hayo. Kwa jumla alikuwa mtetezi wa lugha za asili kama nyenzo ya kukuza lugha ya Kiswahili.

**4.0 Mwana utamaduni**

Hayati Prof. Zacharia Mochiwa alithamini utamaduni wa Kizigua na kama Mtanzania – Utamaduni wa Mtanzania. Kwa kutambua kuwa lugha ni kioo cha utamaduni, alitetea sana Kiswahili na mchango wa lugha za asili katika kuendeleza Kiswahili. Hivyo basi mbali na kulitumikia BAKITA aliwahi kufanya kazi pia katika Ukurugenzi wa Maendeleo ya Utamaduni. Alijiunga na ukurugenzi huo Julai 1979 hadi Februari 1980 akiwa Mkuu wa Idara ya Kiswahili na Mkuzaji Lugha katika Wizara ya Utamaduni na Vijana.

Profesa Mochiwa alithamini utamaduni wake kwa vitendo. Hakuacha jadi, desturi na mila (zilizo nzuri). Ndiyo maana alipenda kusherehekea harusi za wanawe nyumbani alikozaliwa (Sindeni) kwenye mizizi ya utamaduni wa Kizigua. Hakuamini kuwa mtoto anaweza kukua na kulelewa katika maadili mema kwa kukaa mjini tu na kushiriki masuala ya kimjini mjini bila kupitishwa katika desturi na mila za asili. Hivyo alijitahidi kuwalea watoto wake sita (6) katika maadili mema na ndivyo walivyo watoto wake pia na mke wake. Ikumbukwe kuwa Prof. Mochiwa alipata bahati ya kufundisha "Shule ya

Kimataifa ya Tanganyika" (*International School of Tanganyika*) mwaka 1993-1998. Huku kulikuwa na marupurupu mengi ikiwemo watoto wake kusoma pale bure, kama si bure basi kwa gharama nafuu. Lakini hakufanya hivyo. Alichelea watajifunza adabu na tabia mbaya hata kuiga utamaduni wa nje ambao hakuacha kuukosoa kila alipopata fursa ya kutoa maoni yake. Kama kuna jambo lililomkera ni tabia za wanafunzi wa shule hii ya kimataifa ya kuingia madarasani na vikopo ya soda na mikate halafu kuweka miguu juu ya madawati wakati mwalimu anafundisha. Familia yake yote ilikuwa mfano wa kuigwa kwa tabia njema.

**5.0 Profesa, Mwenyekiti wa BAKITA**

Prof. Mochwia aliteuliwa kuwa Mwenyekiti wa BAKITA mwaka 2003 hadi 2006. Hiki kilikuwa kipindi kingine tena ambapo Profesa alipata nafasi ya kukitumikia Kiswahili kwa karibu zaidi. Kama kiongozi na kwa kuelewa uzito wa wadhifa aliopewa na Rais, alijitahidi sana kuhakikisha kuwa majukumu yaliyopangiwa BAKITA yanatekelezwa. Alikalia kiti cha uenyekiti kwa uangalifu na woga mkubwa sana. Hivyo alipenda uwazi na kwa kadri ilivyowezekana kufahamishwa shughuli zote ambazo seketaria ilikusudia kuzifanya. Mwanzoni ilikuwa vigumu kumuelewa, na menejimenti ilimwogopa sana kwa ukali huu. Lakini baadaye ilielewa kuwa ukali huu ulikuwa umekusudiwa kujenga na si kubomoa. Hatimaye menejimenti ilijitahidi kufuata maelekezo yake kila ilipobidi.

Hivyo alikuwa kiongozi mkali, asiyetaka mchezo wala ubabaishaji. Alikuwa mcheshi na mtu mwenye mzaha lakini sio wakati wa kazi. Alikuwa mshauri mzuri katika kazi na katika masuala ya kifamilia. Hakuwa na woga wa kutoa mawazo yake, jambo alilolifanya kwa uadilifu mkubwa, hasa ilipobidi kuzungumza na kutoa hoja mbele ya viongozi wenye dhamana serikalini.

Wadhifa wa uenyekiti haukumfanya aache kushiriki katika kazi nzito za kitaaluma za vipindi vya redio na televisheni. Alishiriki katika vipindi vya BAKITA vya *Lugha ya Taifa* na vya televisheni. Mpaka kufa kwake alikuwa mshiriki katika Kipindi cha *Ulimwengu wa Kiswahili* cha BAKITA kinachotolewa katika TBC, Taifa. Mchango wake katika vipindi vya redio ulianza tangu mwaka 1978, katika vipindi vya "Ngano za Ushairi," na mwaka 1976 "Mtu Chake" na "Utamaduni Wetu". Vipindi vyote hivi vilijenga lugha ya Kiswahili, kutokana na mijadala yake mizito, anuai na ya kina.

**6.0 Padri Zacharia Mochiwa**

Prof. Zacharia aliamini kuwa maisha ya binadamu yamegawanyika katika sehemu mbili. Maisha ya kiroho yanayojengwa na dini na maisha ya kimwili

kama hayo ya uprofesa. Alijiunga rasmi na kazi hiyo ya Upadri mwaka 2002. Kazi ya kumtumikia Mungu ilikuwepo katika damu yake kabla ya mwaka 2002.

Hivyo mbali na kuwa mwanataaluma Prof. Mochiwa alikuwa Padri wa Kanisa la Anglikana akiendesha misa katika kanisa la Mt. Albano la jijini Dar es Salaam. Alikuwa mtumishi mwaminifu aliyedhihirisha matendo yake kwa kujenga kanisa kutokana na fedha zake. Alijenga kanisa kijijini kwake Sindeni, wilayani Handeni, katika mkoa wa Tanga.

Padri Mochiwa hakujua anajiandalia nyumba yake. Alizikwa katika kanisa lake hilo alilojenga. Kufuatana na taarifa ya Askofu Andrew Baji wa Dayosisi ya Tanga, ni marehemu wachache sana katika historia ya Kanisa la Anglikana waliozikwa ndani ya kanisa. Mtu kuzikwa ndani ya kanisa ni ishara ya heshima kubwa kwa marehemu huyo na kwa Mungu aliyekuwa anamtumikia. Ibada ya mazishi yake ilihudhuriwa na makasisi na mashemasi takribani 35 kutoka Tanzania Bara na Visiwani. Aliyeongoza ibada ya mazishi alikuwa Askofu wa Dayosisi ya Mkoa wa Tanga Askofu Andrew Baji. Kufuatana na maelezo ya askofu Baji vigezo vilivyotumiwa kufikia uamuzi huu vimetokana na huduma za kazi zake.

Kama tulivyoeleza Padri Mochiwa alijitolea kujenga kanisa la Anglikana la kijijini kwake Sindeni. Mbali na kanisa hilo alilolijenga kwa fedha yake, alisaidia na kusimamia ukarabati wa Kanisa la Kwachaga, Kata ya Mkata Wilayani Handeni, na Kanisa la Anglikana Mlandizi Wilayani Kibaha. Alichangisha pesa kwa watu mbalimbali zilizowezesha makanisa haya kukarabatiwa na kujengwa. Padri Mochiwa alikuwa mpenzi wa watu asiyependa makuu. Kutokana na unyenyekevu wake alipewa kiti cha Simon Mkirene. Hiki kilikuwa cheo maalumu katika uongozi wa Kanisa Anglikana.

Kujitoa kwake hakukuishia katika ujenzi na ukarabati wa makanisa bali katika kusaidia watumishi wa Mungu. Alisaidia kumsomesha mwanafunzi mmoja katika chuo cha Biblia cha Anglikana. Vilevile alilipa mshahara wa mtumishi mmoja wa Mungu. Huduma zote hizi alizifanya kutokana na fedha zake. Hata mwandishi wa makala hii amewahi kulipiwa ada ya masomo wakati akijiandaa kwenda kusoma digrii yake ya udaktari huko Marekani na hakudaiwa kitu. Mbali na kumtafutia nafasi ya masomo, alitumia fedha yake kuhakikisha kuwa anakwenda kusoma, na alimtia moyo asome hadi shahada ya udaktari. Alipenda maendeleo ya kielimu. Hivyo alijitolea kwa hali na mali ili jamaa na ndugu zake waweze kusoma na kujiendeleza. Hakuonesha ubaguzi wowote ulipohitajika msaada wa kifedha.

Huyu ndiye aliyekuwa Profesa Padri Zacharia Salimu Marko Mochiwa. Amefariki dunia wakati ulimwengu wa Kiswahili ukimhitaji. Kwa Wakristo wa Anglikana amefariki wakati utumishi wake kiroho unahitajika. Basi tuseme nini

kuhusu Profesa, Padri Zacharia Mochiwa. Ni mengi aliyotuachia ya kutufundisha jinsi ya kumaliza siku zetu zilizobakia hapa duniani.


***Machapisho mapya ya TATAKI na bei zake:***

Stadi za Lugha ya Kiswahili

**UFAHAMU NA UFUPISHO 1**

*Bei sh.5,000.00*

Stadi za Lugha ya Kiswahili

**UTUNGAJI 2**

*Bei Sh.5,000.00*

Stadi za lugha ya Kiswahili

**SARUFI 1**

Bei Sh. 5,000.00


*******************************************